**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAREJEO NA. 241 YA 2022**

**EDWARD L. MMBAGA ................................... MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**FMJ HARDWARE LTD ................................... MJIBU MAOMBI**

*(Kutokana na Uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Kanda ya DSM - Ilala)*

(Chacha: Muamuzi)

Tarehe 30.05.2022

Katika

**CMA/DSM/ILA/424/21/166/21**

==============================

**HUKUMU**

**03.10 & 13.12.2022**

**Rwizile, J**

Haya ni maombi ya marejeo. Mleta maombi anaomba Mahakama, kuitisha, kupitia na kutengua uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Tume) uliotolewa tarehe 30.05.2022.

Maelezo ya mgogoro huu kwa ufupi ni kwamba, Mleta maombi aliajiriwa na mjibu maombi kama meneja mauzo kwa mkataba wa mwaka mmoja. Hata hivyo, mkataba huo ulisitishwa tarehe 29.07.2021, kwa kile kilichoelezwa ni kufika ukomo.

Mleta maombi hakuridhika na uamuzi wa mwajiri na akafungua shauri mbele ya Tume akidai kuvunjwa makataba wake.

Baada ya Tume kusikiliza pande zote mbili, iliona mgogoro wake haukuwa na mashiko, hivyo ikaufukuza. Mleta maombi hata hivyo hakuridhika, akaamua kufungua maombi haya ya marejeo.

Katika maombi yake ameeleza sababu zake kama ifuatavyo: -

i. *Kwamba, mwamuzi alijiongoza vibaya kisheria kwa kushindwa kuzingatia mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye ushahidi uliotolewa na upande wa mlalamikaji na mlalamikiwa hakuupinga.*

ii. *Kwamba, mwamuzi alijiongoza vibaya kisheria kwa kutozingatia maelezo ya awali ya mleta maombi, ambapo mjibu maombi alikubaliana na maelezo ya awali ya mleta maombi kuwa mleta maombi aliajiriwa kama meneja manunuzi kuanzia 06.04.2020 mpaka 05.04.021.*

iii. *Kwamba, mwamuzi alijiongoza vibaya kisheria kwa kutozingatia mkataba wa ajira wa mlalamikaji ambao upo kwenye maelezo ya awali ya mleta maombi, ambao mjibu maombi aliukubali kwenye maelezo yake ya awali, ila mwamuzi alijikita kwenye mkataba wa kufoji ambao ulikuwepo kwenye mlolongo wa nyaraka za*

Labour Court TZ.

*nyongeza za mjibu maombi ambazo hazikuwepo kwenye maelezo ya awali ya mlalamikiwa.*

*iv.* *Kwamba, mwamuzi alijiongoza vibaya kisheria kwa kukubali ushahidi wa Dw1 katika ukurasa 3, aya ya mwisho nakusema kwamba mlalamikaji aliajiriwa kama wakala, kinyume na kwamba mjibu maombi kwenye maelezo yake ya awali alikubali kuwa mlalamikaji aliajiriwa kama meneja manunuzi.*

*v.* *Kwamba, mwamuzi alijiongoza vibaya kwa kuandika ushahidi wake binafsi wakutengeneza dhidi ya malalmikaji katika ukurasa wa 5 aya 2 ya Tuzo kwamba mkataba wa Pw1 unaishia 31.08.2021 ili kuhalalisha mkataba feki wa mlalamikiwa ambao ulikuwa kwenye mlolongo wa nyaraka za nyongeza za mlalamikiwa.*

*vi.* *Kwamba, mwamuzi alitoa Tuzo isiyokuwa ya haki bila kuzingatia kuwa mlalamikiwa alivunja mkataba wa ajira wa mlalamikaji bila kufuata sheria.*

Kila upande uliwakilishwa na mawakili wasomi. Mleta maombi aliwakilishwa na Bwana Deo Ukani Ngusaru na mjibu maombi aliwakilisha na Bwana Edwin Somoka Nkalani.

Labour Court Tz.

Katika mawasilisho yake, wakili wa mleta maombi Bwana Ngusaru alieleza kuwa mleta maombi aliajiriwa kwa mkataba wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 06.04.2020 hadi 05.04.2021 (kielelezo P1). Aliendelea kueleza kuwa mjibu maombi katika maelezo yake ya awali alikubalia ajira ya mleta maombi lakini baadae alifikisha mkataba mwingine unaoonyesha kuwa mleta maombi aliajiriwa tarehe 01.09.2020 kwa mwaka mmoja uliotakiwa kuisha tarehe 31.08.2021 (kielelezo D1).

Alisema kuwa Tume iliukataa mkataba wa mleta maombi bila ya sababu na haikuuzingatia. Akaeleza zaidi kuwa mleta maombi alifanya kazi kwa mjibu maombi zaidi ya miezi minne hadi tarehe 29.07.2021 alipoachishwa kazi. Kwa mtazamo wake mkataba wa mleta maombi ulihuishwa kwa kipindi hicho na uthibitisho ni malipo yake ya mshahara (vielelezo P2 na P3).

Bwana Ngusaru alisema, mjibu maombi alieleza kuwa aliajiriwa kama karani na sio afisa manunuzi kitu ambacho hakikupingwa katika maelezo. Hivyo akaiomba Mahakama itengue uamuzi wa Tume na kuruhusu mleta maombi kulipwa stahiki zake.

Katika majibu, Bwana Nkalani aliwasilisha kuwa nyaraka iliyopokelewa mbele ya Tume kama P1 ilikuwa ni "offer" ila mkataba wa ajira ulipokelewa kama kielelezo D1. Akiendelea kueleza, alisema kuwa hakuna

labourcourt TZ

ushahidi wowote ulifikishwa mbele ya Tume kuonyesha kuwa kielelezo D1 ni cha kughushi na kuwa hoja hiyo imeibuliwa mbele ya Mahakama katika kiapo.

Aliendelea kuwasilisha kuwa mleta maombi alipewa taarifa ya kutokuwa na nia ya kuendelea naye na kielelezo hicho kilipokelewa na Tume. Akaeleza, kanuni ya 24(2) ya Kanuni ya *Labour Institutions (Medition and Arbitration Guidelines)* Rule, Tangazo la Serikali Na. 67 ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa maelezo ya awali sio ushahidi hadi pale ambapo upande wa pili utayakubali. Alibainisha kuwa mkataba wa mleta maombi haukuhuishwa na wala haikujadiliwa na Tume, bali kulikuwa na hoja ya kufukuzwa kazi isivyo halali.

Katika mawasilisho ya nyongeza Bwana Ngusaru pamoja na kurejea yale aliyoyawasilisha katika wasilisho la awali alisisitiza kuwa mleta maombi aliajiriwa kama afisa manunuzi.

Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, Mahakama inaona hoja tatu hapa chini zinahitaji kuamriwa: -

*i.* *Kama maelezo ya awali ni sehemu ya ushahidi,*

*ii.* *Upi ni mkataba halali kati ya kielelezo P1 na kielelezo D1,*

*iii.* *Kama mkataba ulivunjwa isivyo halali*

Katika hoja ya kwanza Mahakama inakubaliana na wakili wa mjibu maombi kuwa maelezo ya awali sio ushahidi hadi pale pande zote mbili zitakapokubaliana nayo na endapo yatathibitishwa na ushahidi. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 24(2) ya TLS Na. 67 la mwaka 2007 na pia imeamriwa katika kesi ya **Fredy Ngodoki v Swissport Tanzania PLC**, Civil Appeal No. 232 of 2019, Court of Appeal of Tanzania. Hivyo Tume ilipoacha kuzingatia maelezo ya awali yaliyotolewa katika kuchambua ushahidi wake ilikuwa sahihi. Hoja ya mleta maombi katika hili, haina mashiko.

Katika hoja ya pili Mahakama imepitia vielelezo vilivyofikishwa mbele ya Tume na kubaini kuwa kielelezo P1 kuwa ni "Offer of Employment". Nyaraka hii inaonyesha dhahili kuwa lengo lake lilikuwa ni kuonyesha nia ya kutaka kumwajiri mleta maombi. Kwani "offer" hiyo imeeleza wazi kuwa ajira ya mleta maombi itaanza baada ya kuweka sahihi katika mkataba wa ajira. Kwa rahisi ya rejea inasema: -

> *"Dear Edward,*
>
> ***Re: <u>Offer of Employment</u>***
>
> *... Your employment will be effected under the terms and conditions stated hereunder and you will be expected to sign an employment contract with FMJ Hardware immediately upon hire:"*

Hivyo "offer" hiyo imedhihirisha wazi kuwa haukuwa mkataba. Katika kielelezo D1 inaelezwa wazi kuwa ni "MKATABA WA MUDA MAALUMU", kwa mantiki hiyo muamuzi alikuwa sahihi alipobainisha kuwa mkataba unaowaongoza mleta maombi na mjibu maombi ni ule uliopokelewa kama kielelezo D1. Hivyo hoja ya pili ni kama ilivyoamriwa na Tume.

Katika hoja ya tatu

Baada ya Mahakama kubaini kuwa mkataba halisi ni ule wa kielelezo D1 uliupitia na kubaini kuwa mkataba huo ulikuwa ni wa muda maalumu wa mwaka mmoja. Mkataba ulianza tarehe 01.09.2020 na kutakiwa kuisha tarehe 31.08.2021. Hivyo tarehe 29.07.2021 mleta maombi alipatiwa na mjibu maombi barua ya nia yake ya kutohuisha mkataba huo ifikapo tarehe 31.08.2021.

Kama sheria inavyoelekeza, mkataba wa ajira ya muda maalum unahesabika kuisha pale ambapo muda wake unapofikia kikomo. Hayo yanaelezwa katika kanuni ya 4(2) ya *Employment and Labour Relations (Code of Good Practice)* TLS Na. 42 ya mwaka 2007. Hivyo kwa kitendo cha mjibu maombi kumwandikia mleta maombi taarifa ya nia yake ya kutokukusudia kuuhuisha ililikuwa ni kumtaarifu mleta maombi ili afahamu nia hiyo. Kwa sababu hiyo inaonyesha dhahili kuwa mkataba baina ya

Labour Court TZ.

mleta maombi na mjibu maombi ulisitishwa kutokana na muda wake kufika mwisho.

Mahakama haya baada ya kupitia maombi ya marejeo inaona kwamba maombi yaliyowasilisha kutokuwa na mashiko. Hivyo yametupiliwa mbali. Na kwakuwa huu ni mgogoro wa kikazi, kila upande utajilipia gharama zake.

**A.K. Rwizile**

**JUDGE**

**13.12.2022**

Labour Court Tz.